KANUNI ZA BUNGE

ZIMETUNGWA KULINGANA NA KATIBA YA MUHASSO

SEHEMU YA KWANZA

1. Kanuni hizi za bunge (USRC) ni toleo la mwaka 2014

(i) Katika kanuni hizi isipokuwa kama maelezo yatahitajika vinginevyo

"Bunge" maana yake ni chombo cha uwakilishi wa wanafunzi (USRC) kulingana na katiba ya MUHASSO

''Mbunge' maana yake ni mwakilishi yoyote wa wanafunzi (USRC) kama ilivyoelezwa na katiba ya MUHASSO

'Katibu' maana yake katibu wa Bunge.

'Waziri Mkuu' maana yake waziri mkuu wa MUHASSO.

"Hoja ya kamati" maana yake ni hoja inayotokana na majadiliano ya kamati yoyote ya Bunge.

"Hoja ya Mbunge" maana yake ni hoja inayotolewa na mbunge asiyekuwa waziri

''Katiba'' maana yake ni katiba ya MUHASSO.

(ii) Bila kuathiri masharti ya katiba, kanuni hizi zitatumika katika uendeshaji wa shughuli zote za Bunge.

SEHEMU YA PILI

UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA BUNGE

2. (1) Kutakuwa na Spika wa Bunge, ambaye ambaye atachaguliwa na wabunge na

atashika madaraka yake kufuatana na masharti ya katiba na kanuni hizi.

(2) Wakati wowote ambapo Spika, kutokana na kutokuwapo chuoni au sababu nyingine yoyote hatoweza kutekeleza madaraka au majukumu yake, basi madaraka au majukumu yake yatatekelezwa na Naibu Spika na kama Naibu Spika hayupo basi majukumu hayo yatatekelezwa na Wenyekiti wa Bunge, au mbunge yeyote ambaye si waziri na atachaguliwa ndani ya kikao cha bunge kwa kipindi chote ambacho Spika hatokuwepo.

3. (1) Spika atakuwa ndiye kiongozi wa Bunge na ataliwakilisha Bunge katika shughuli na vikao vingine vyote nje ya Bunge.

(2) Spika ataongoza kila kikao cha Bunge na ndiye mwenye mamlaka ya kuamua mambo yanayoweza kuzungumzwa bungeni akishirikiana na Wenyeviti wa Bunge na Ofisi ya Mshauri wa Wanafunzi.

(3) Spika atawajibika kutilia nguvu kanuni zote za Bunge, na endapo mbunge yeyote hakuridhika na utiliaji nguvu wa kanuni hizi basi atawasilisha malalamiko yake kwa mwenyekiti wa kamati ya kanuni za bunge ambayo itatakiwa ikutane mara moja ili kuweza kutoa uamuzi wake kwa spika juu ya jambo hilo, na Spika atalijulisha Bunge uamuzi uliotolewa.

4. (1) Spika wa bunge ataondolewa kulingana na katiba ya MUHASSO.

(2) Baada ya mgombea wa kiti cha Spika kutangazwa mshindi ataapishwa kiapo cha uaminifu.

5. (1) Kutakuwa na Naibu Spika ambaye atachaguliwa na wabunge ambaye atakuwa ndiye msaidizi wa Spika na atatekeleza majukumu yote ya Spika pale ambapo

Spika atakuwa hayupo.

(2) Naibu Spika ataondolewa kulingana na Katiba ya MUHASSO.

6. (1) Kutakuwa na wenyeviti wawili wa bunge ambao watachaguliwa na wabunge kutoka miongoni mwa wenyeviti wa kamati za kudumu za bunge.

(2) Uchaguzi wa Wenyeviti wa bunge utafanyika kwa kufuatana utaratibu kwamba karatasi ya kura itakuwa na majina ya wenyeviti wote wa kamati za kudumu. Kila mbunge atapiga kura ya kuchagua jina moja katika orodha hivyo. Wagombea wawili watakaokuwa wamepata kura nyingi zaidi kuliko wenzao, ndio watakaokuwa wamechaguliwa kuwa wenyeviti wa Bunge.

(3) Mwenyekiti wa Bunge ataondolewa kwa kufuata utaratibu wa Kikatiba wa kumwondoa Spika madarakani.

7. Waziri mkuu atakuwa ndiye kiongozi wa shughuli za serikali bungeni kama hataweza kuwepo bungeni, atamteua waziri yeyote kuwa kiongozi wa shughuli za serikali bungeni.

8. (1) Kutakuwa na Katibu wa bunge ambaye atawajibika kuhakikisha utekelezaji bora wa shughuli za bunge na madhumuni hayo.

a) Atahudhuria vikao vyote vya bunge na kama akiagizwa na spika vikao vya kamati nyingine vyote vya bunge.

b) Atatayarisha taarifa rasmi kwa mujibu wa kanuni hizi.

c) Atatayarisha ripoti ya shughuli za Bunge na kuhifadhi ikiwa inaonyesha

(i) Maagizo yote yaliyotolewa na Bunge

(ii) Shughuli zote zilizopangwa kufanywa siku yoyote ya baadae.

(iii) Taarifa zote za maswali na hoja zilizojibiwa Bungeni

(2) Katibu atahakikisha utunzaji mzuri wa kumbukumbu za Bunge na vielelezo vingine vilivyowasilishwa Bungeni

(3) Mbunge yeyote anaweza kukagua kumbukumbu na vielelezo hivyo wakati wowote unaofaa, na vilevile watu wengine wanaweza kuzikagua kumbukumbu hizo kwa kufuata utaratibu utakaowekwa na Spika.

(4) Katibu atawajibika kuhakikisha kuwa ukumbi wa mkutano na mazingira yake pamoja na vifaa vingine vinavyohusika na shughuli za Bunge, viko katika hali inayofaa kuliwezesha bunge kutekeleza wajibu wake ipasavyo

(5) Katibu wa bunge atachaguliwa na kikao halali cha Bunge bila kuathiri katiba na masharti ya kanuni hizi.

9. Kutakuwa na Ofisi ya Bunge itakayo tumiwa na wabunge na kamati kwa kuzingatia utaratibu utakaoagizwa na Spika au utakaowekwa na Bunge.

SEHEMU YA TATU

10 (1) Bila kuathiri masharti ya Katiba, Mkutano wa kwanza wa Bunge Jipya utaanza tarehe na saa ile ambayo Bunge jipya limeitishwa na Rais kukutana.

(2) bila ya kuathiri masharti ya kanuni hizi kuhusu kuanza na kufungwa kwa vikao vya Bunge, Mkutano wa kwanza wa bunge utaendelea kukutana kwa muda wote na utahitajika kutekeleza na kukamilisha shughuli zote za mkutano wa kwanza wa Bunge jipya.

11 (1) Shughuli za mkutano wa kwanza wa Bunge jipya zitakuwa kama ifuatavyo:

(a) Uchaguzi wa Ofisi ya Spika.

(b) Kiapo cha uaminifu kwa Ofisi ya Spika na wabunge wote.

(c) Ripoti ya serikali iliyokuwepo madarakani itakayosomwa na aliyekuwa Waziri Mkuu.

(d) Kukabidhi Ofisi kwa Serikali mpya.

(e) Hoja ya kujadili hotuba ya Rais.

12 (1) Mikutano yote ya Bunge itafanyika kama itakavyokuwa imepangwa kwenye Almanac ya Chuo ya mwaka wa masomo.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kanuni hizi endapo manufaa ya wanafunzi yatahitajika kuwa Bunge lisikutane tarehe ile iliyowekwa kwa mkutano, bali likutane tarehe ya mbele zaidi au nyuma zaidi, basi Spika anaweza kufanya hivyo, baada ya kushauriana na Kiongozi wa shughuli za serikali Bungeni, kisha kuitisha Bunge likutane tarehe hiyo ya mbele zaidi au nyuma zaidi.

(3) Iwapo tarehe ya kukutana itakuwa mbele zaidi ya ile iliyowekwa, basi tarehe hiyo mpya haitakuwa mbele zaidi ya siku kumi na nne (14) kutoka tarehe ya kikao iliyopangwa, basi Spika ataliita Bunge likutane kwa dharura.

(4) Endapo wabunge wasiopungua nusu ya idadi ya wabunge wote watapeleka kwa Spika kwa maandishi ombi lililowekwa saini na wabunge hao, la kutaka Bunge liitishwe kwa dhararu kabla ya tarehe ya kikao iliyopangwa, basi Spika ataliita Bunge likutane kwa dharura.

13 (1) Mkutano wa Bunge utaanza saa mbili asubuhi siku ya Jumamosi, ila tu kama Bunge litaamua vinginevyo au kama litakutana kwa dharura.

(2) Bunge litandelea kukutana mpaka saa saba mchana ifikapo saa hiyo, shughuli yeyote itakayokuwa inafanyika itasitishwa, isipokuwa kama Bunge litaikubali hoja ya kuendelea kukutana kwa muda utakaotajwa, kama shughuli hiyo itasitishwa basi Spika bila kuwahoji Wabunge ataamua lisitishwe mpaka saa nane ambapo shuguli hiyo itaendelea.

14 (1) Kila mkutano wabunge utafungwa kwa kuliahirisha bunge hadi mkutano utakaofuata.

(2) Endapo shughuli zote zilizowekwa kwenye agenda zimemalizika, hoja ya kuahirisha Bunge itataja siku na saa ambayo mkutano utakaofuata utaanza.

SEHEMU YA NNE

SHUGHULI ZA BUNGE

15 (1) Katika kuhakikisha uwazi katika serikali kutakuwa na ripoti ya utendaji ya serikali itakayosomwa na ofisi ya waziri mkuu kikao kimoja kabla ya Bunge kuvunjwa.

(2) Hoja ya kujadili ripoti ya waziri mkuu.

16. (1) Rais anaweza kulihutubia bunge siku yoyote ambayo bunge linakutana.

(2) Wakati wa kuanza mkutano wowote wa Bunge,

(a) Kama spika atalitangazia bunge ni wakati gani Rais atafanya hivyo.

(b) Baada ya hotuba ya Rais spika atatenga muda kwa ajili ya kuijadili hotuba ya Rais.

(3) Shughuli za Bunge katika kila kikao zitaendeshwa kwa utaratibu ufuatao

(a) Kusoma na kupitisha Agenda

(b) Taarifa ya Rais.

(c) Taarifa ya Spika

(d) Maswali ambayo taarifa zake zimetolewa

(e) Hoja za kuahirisha shughuli ili kuyajidili mambo muhimu ya dharura

(f) Kauliza mawaziri

(g) Maelezo binafsi ya wabunge

(h) Hoja au taarifa za kamati

(i) Hoja binafsi za wabunge

(5) Taarifa ya agenda za kikao cha Bunge itatolewa siku mbili kabla ya kikao ,vinginevyo maelezo yatatolewa juu ya kuchelewa kwa ajenda.

(4) Shughuli za Bunge katika kila kikao zitatekelezwa kwa kufuata jinsi zilivyowekwa katika agenda za siku hiyo, au kwa kufuata utaratibu mwingine ambao Spika ataagiza ufuatwe kwa ajili ya uendeshaji bora wa shughuli za Bunge.

17 (1) Mbunge yeyote anaweza kuwasilisha Bungeni maombi yeyote juu ya jambo lolote kwa niaba ya watu wanaotoa ombi hilo, taarifa ya ombi hilo iwe imetolewa na kupokelewa na Spika siku mbili kabla ya mkutano ambapo ombi linakusudiwa kutolewa.

(2) Mbunge anayewasilisha ombi atatoa maelezo mafupi ya kuwatambulisha watu wanaotoa ombi hilo, idadi yao, saini zilizoambatanishwa kwenye ombi hilo sambamba na madai ya msingi na madhumuni ya ombi hilo.

18. (1) Waziri anaweza kuulizwa maswali yoyote ya jamii au jambo lingine lolote linalosimamiwa na wizara au ofisi yake. Vile vile Mbunge yeyote anaweza kuulizwa maswali kuhusu mambo yoyote anayohusika nayo kutokana na kuteuliwa na wabunge kushughulikia mambo hayo.

(2) Madhumuni ya swali lolote yatakuwa ni kutaka kupewa habari kuhusu jambo mahususi

ambalo waziri au mbunge huyo anahusika au anawajibika na kutaka kusisitiza hatua fulani ichukuliwe au wajibu utekelezwe.

19. (1) maswali yanaweza kuulizwa endapo masharti yafuatayo yatazingatiwa

(a) Swali halitamtaja mtu yeyote kwa jina au kutoa maelezo yoyote mahususi ila tu kama ni lazima kufanya hivyo ili swali lieleweke.

(b) Endapo swali lina maelezo yoyote mahususi mbunge anayeuliza swali hilo atawajibika kuhakikisha kuwa maelezo hayo ni sahihi, vinginevyo habari za kusikika bila vithibitisho hazitakubaliwa.

(c) Swali halitokuwa na mambo zaidi ya mawili na lisiwe refu kupita kiasi, lisiwe na maelezo ya dhihaka, maoni masingizio, sifa zisizo za lazima, au kutegemea habari za kubahatisha tu.

20. (1) Mbunge anayeuliza swali atasimama mahali pake baada ya kuchaguliwa na Spika, waziri au mbunge aliyeulizwa swali atajibu papo hapo

(2) Waziri aliyeulizwa swali atakuwa na wajibu wa kulijibu swali hilo kwa uangalifu kama alivyoulizwa.

21. Mbunge yeyote ataweza kutoa hoja Bunge lisitishe mjadala ili kujadili jambo halisi.

22. (1) Waziri anaweza kutoa kauli bungeni kuhusu jambo lolote ambalo serikali inawajibika.

(2) Mbunge yoyote anaweza kutoa maelezo yake binafsi bungeni lakini atapaswa kuhakikisha maelezo yake hayo hayakiuki kanuni yoyote ya Bunge.

SEHEMU YA TANO

KANUNI ZA MAJADILIANO

23. (1) Mbunge akitaka kusema atanyoosha mkono wake juu na Spika atamruhusu azungumze.

(2) Kila mbunge atasema akiwa amesimama na atatoa maelezo yake akimwelekea Spika isipokuwa wabunge ambao kutokana na mahitaji maalum hawawezi kuzungumza wakati wamesimama.

(3) Mbunge hataruhusiwa kujibizana na mbunge mwingine anayeuliza au anayejibu swali.

24 (1) Mbunge hatazungumzia jambo lolote ambalo yeye mwenyewe ana maslahi ya kifedha nalo, isipokuwa baada ya kutaja jinsi anavyohusika na namna ya maslahi hayo.

(2) Katika mjadala wowote, mawaziri watatajwa kwa kutumia majina ya nyadhifa zao na Wabunge watatajwa kwa kutumia neno "Mheshimiwa" kabla ya majina yao.

25. (1) Kila mbunge anawajibika kujali muda ili kuwawezesha wabunge wengine zaidi kupata nafasi ya kuchangia mawazo yao.

(2) Mbunge hataruhusiwa kurudiarudia jambo ambalo limeshazungumzwa katika muda wa maswali ya msingi.

26. (1) Ni marufuku kabisa kusema uongo bungeni, kwa sababu hiyo mbunge anapokuwa akisema Bungeni, Bunge litawajibika kuwa na uhakika kwamba maaelezo anayoyatoa ni sahihi na siyo mambo ya kubuni au ya kubahatisha tu, na Spika au Mbunge mwingine yeyote anaweza kumdai Mbunge huyo atoe uthibitisho wa usemi wake kwa muda utakao kuwa umewekwa na Spika

(2) Ni marufuku kwa Mbunge yeyote;

a) Kutumia lugha ya matusi

b) Kumsingizia Mbunge mwingine au kumshambulia binafsi, isipokuwa kwa kutoa hoja mahususi inayohusu mwenendo wa Mbunge huyo.

c) Kujiingiza katika mambo ya kuwasema wenzake au kuleta mgawanyiko ndani ya Bunge.

27. (1) Mbunge aliyepo bungeni wakati wa mjadala;

a) Atatulia na kukaa kwa heshima mahali pake, na hata tangatanga katika ukumbi wa mkutano bila sababu ya msingi.

b) Hatasoma kitabu chochote gazeti au barua ila tu kama yahusu shughuli za mjadala wakati huo.

c) Mbunge yeyote haruhusiwi kuongea na simu au kuchezea simu ndani ya ukumbi wa mkutano.

28. (1) Mbunge anayesema hatakatizwa usemi wake na Mbunge mwingine isipokuwa jambo linalohusu utaratibu. Lakini Mbunge mwingine anayetaka kumkatiza kwa ajili ya kutoa taarifa ya ufahamisho juu ya jambo lilowekwa vibaya kwa Mbunge huyo anayesema.

29. (1) Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema, na kuomba "mwongozo" wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea haliruhusiwi kwa mujibu wa kanuni na taratibu za Bunge.

SEHEMU YA SITA

AMANI NA UTULIVU BUNGENI

30. (1) Spika atawajibika kuhakikisha kuwa utaratibu bora unafuatwa Bungeni na uamuzi wake kuhusu jambo lolote la utaratibu utakuwa ni wa mwisho.

(2) Mbunge yeyote atakayekiuka utaratibu au kanuni za Bunge anaweza papo hapo kutakiwa na Spika afuate utaratibu na vilevile Mbunge yeyote anaweza kusimama na kumfahamisha Spika kwamba kuna Mbunge anayekiuka utaratibu.

31. (1) Mbunge anayeshikilia kusema mambo ambayo haruhusiwi na kanuni hizi anaweza kuamriwa na Spika akatishe hotuba na kukaa mahala pake.

(2) Iwapo Mbunge yeyote atatumia maneno au lugha isiyotakiwa Bungeni, kwa mfano lugha ya matusi, ya uchokozi au ya kumuudhi Mbunge mwingine na kama akitakiwa kujirekibisha kwa kufuta usemi wake huo, iwapo atasita au kukataa kufanya hivyo basi Spika anaweza kumwamuru Mbunge huyo atoke nje ya ukumbi wa mkutano na abaki nje kwa muda wote uliosalia wa kikao.

32. Mbunge yeyote atakaye chukuliwa hatua na Bunge ama ya kusimamishwa au kufukuzwa Bungeni atapoteza haki zote za ubunge mpaka pale atakapo rejeshwa Bungeni.

33. Wabunge wote ni lazima wawe na vitambulisho vyenye majina na uwakilishi wao na watahitajika kuvionyesha wakati wa mikutano yote ya Bunge.

34. Kwa madhumuni ya kudhibiti fujo endapo itatokea ndani ya mkutano, Spika anaweza kuahirisha Bunge bila hoja kutolewa au kusimamisha kikao kwa muda ambao atautaja mpaka hali ya amani na utulivu itakapojirudia katika ukumbi wa mkutano.

SEHEMU YA SABA

UHALALI WA SHUGHULI

35. Kiwango cha mikutano na vikao vyote vya Bunge wakati wa kufanya maamuzi kitakuwa ni 1/3 ya wabunge wote, kama katiba inavyoonyesha.

36. (1) (a) Mambo yanayohitaji kuamuliwa na Bunge yaamuliwe kwa kufuata maoni ya wabunge walio wengi waliohudhuria na kupiga kura bungeni.

(b) Spika au Mwenyekiti wa Bunge, wakati anapokuwa amekalia kiti cha Spika, hatakuwa na kura ya kawaida bali atakuwa na kura ya uamuzi, endapo kura za ndiyo na siyo zitalingana.

(c) Wakati wa upigaji kura juu ya jambo fulani Spika atataka uamuzi kwanza kwa watu wanao afika waseme ndiyo kisha atataka wale wasio afiki waseme siyo.

(d) Iwapo mbunge yeyote atadai kura zihesabiwe basi Spika ataamuru kura zihesabiwe.

(2) Bila kuathiri kipengele cha 36(1) (a-d) maamuzi yoyote yatakayopitishwa na Bunge bila uwepo Ofisi ya Mshauri wa Wanafunzi yatakuwa ni batili.

SEHEMU YA NANE

KAMATI ZA BUNGE

37. (1) Kutakuwa na kamati za kudumu za bunge zitakazoundwa na wabunge wenyewe.

(2) Mbunge yeyote ambaye si waziri ataweza kuteuliwa kuwa mjumbe wa kamati ya kudumu yoyote ambaye inahusika na kanuni hii, waziri mwenye dhamana ya jambo lolote

linaloshughulikiwa au kufikiriwa na kamati pamoja na Naibu Waziri watakuwa wajumbe wa kamati itakapokuwa ina shughulikia jambo hilo.

(3) Uteuzi wa wajumbe wa kamati utazingatia

a) Uzoefu na ujuzi wa mjumbe kuhusu kazi za kamati hiyo..

b) Kwa kadri itakavyowezekana itazingatiwa matakwa ya wabunge wenyewe.

(4) Katibu atahakikisha kuwa wabunge wote orodha ya majina yao kwenye kamati na jinsi walivyoteuliwa.

(5) Wabunge walioteuliwa watashika nafasi zao kama wajumbe wa kamati zao kwa muda ambao wataendelea kuwa wabunge (bila kuwa waziri au Spika)

(6) Wajumbe wa kila kamati watamchagua mwenyekiti kutoka miongoni mwao kwa muda wote ambao atakuwa Mbunge.

(7) Mwenyekiti ataongoza vikao vyote vya kamati endapo mwenyekiti hayupo kwenye mkutano wowote wabunge waliohudhuria watamchagua mmoja wapo miongoni mwao kuongoza mkutano.

(8) Kamati ya kudumu itakutana kila inapoitwa na Spika, au na Mwenyekiti wake baada ya kupata idhini ya Spika kila kamati itafanya vikao vyake kwa kuzingatia bajeti ya kamati hiyo kwa mwaka.

(9) Kiwango cha mkutano wowote wa kamati ya kudumu kitakuwa theluthi moja ya wabunge wote wa kamati.

38. Kutakuwa na kamati za kudumu zifuatazo:

a) Kamati ya mambo ya katiba na sheria idadi ya wajumbe isiyozidi sita.

b) Kamati ya fedha na Hesabu za serikali, idadi ya wajumbe isiyozidi sita.

c) Kamati ya Haki, maadili na madaraka ya Bunge, idadi ya wajumbe isiyozidi sita.

d) Kamati ya mikopo, idadi ya wajumbe isiyozidi sita.

e) Kamati ya Afya na Chakula, idadi ya wajumbe isiyozidi sita.

f) Kamati ya Malazi na Maji, idadi ya wajumbe isiyozidi sita.

g) Kamati ya mazingira na usafi wa jumla, idadi ya wajumbe isiyozidi sita.

h) Kamati ya usawa wa kijinsia na makundi maalum, idadi ya wajumbe isiyozidi sita.

39. (1) Kila kamati ya kudumu itakuwa na jukumu la kufuatilia utekelezaji wa ahadi za serikali katika kutatua matatizo ya wanafunzi, ambazo zinagusa mamlaka ya kamati husika.

(2) Mbali na majukumu ya msingi, kamati yoyote yaweza kupendekeza kwa Spika ipewe majukumu ya nyongeza ambayo yatatajwa katika pendekezo hilo. Hali kadhalika Spika aweza kukaidhi jambo lingine lolote kwa kamati yoyote kama atavyoona inafaa.

40. Kamati teule inaweza kuundwa na Bunge kwa madhumuni maalum, kwa hoja mahususi itakayo tolewa kwa ajili hiyo na kuafikiwa.

(1) Wabunge wataamua idadi ya wajumbe wa kamati teule.

(2) Wajumbe wa kamati teule watamchagua mwenyekiti kutoka miongoni mwao atakayeongoza vikao vyote vya kamati.

(3) Kamati teule itatoa taarifa Bungeni kuhusu maoni na uchunguzi wake pamoja na kumbukumbu za ushahidi uliopelekwa, na vile vile yaweza kutoa taarifa maalum ya mambo yoyote ambayo itaona inafaa bunge liyajue.

(4) Sehemu ya katikati ambayo itatoa maelekezo kamili kuhusu jambo au mambo yote yaliyofanyika uchunguzi na kamati.

(a) Sehemu ya utangulizi ambayo itaonyesha hadidu za rejea ambapo kamati ilipewa, maelekezo yoyote yaliyotolewa kwa kamati, njia au mbinu zilizo tumika na kamati katika kutekeleza majukumu yake, pamoja na mambo mengine, kama yapo ambayo yalijitokeza wakati wa uchaguzi.

(b) Sehemu ya katikati, ambayo itatoa maelekezo kamili kuhusu jambo au mambo yote yaliyofanyika uchunguzi na kamati.

(c) Sehemu ya mwisho, ambayo itatoa maaoni na mapendekezo ya kamati kwa bunge.

SEHEMU YA TISA

UTARATIBU WA KUONDOA VIONGOZI MADARAKANI

41. (1) Bunge lina uwezo wa kumwondoa madarakani kiongozi yoyote

(a) Rais

(b) Waziri Mkuu.

(2) Taratibu zote za kumuondoa kiongozi yeyote madarakani zitafanyika kuendana na katiba

SEHEMU YA KUMI

MENGINEYO

42. Kuhudhuria vikao na mikutano ya Bunge ni wajibu wa kwanza wa kila Mbunge, hivyo Mbunge yeyote atakayeshindwa kuhudhuria vikao viwili vya Bunge bila taarifa rasmi ya maandishi kwa Spika atapoteza Ubunge wake.

43. Shughuli za Bunge zitaendeshwa kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza, bila tafsiri ya lugha hizo kutolewa.

44. (1) Kila Mbunge atawajibika kuvaa mavazi ya heshima ambayo yatahifadhi heshima yake yeye, hadi ya Bunge na chuo kwa ujumla na mavazi hayo yatakuwa kama ilivyoainishwa katika mfumo wa uvaaji wa chuo yani dressing code.

(2) mavazi yasiyo ya heshima ni pamoja na;

a) Kaptula na jinsi

b) Singlet ya kuvaa ndani ya shati.

c) Nguo yoyote inayoonyesha maungo ya mwili (transparent clothes)

45. (1) bunge linaweza wakati wowote, kupitisha adhimio la kufanya mabadiliko katika kanuni

yoyote kutokana na mapendekezo ya kamati ya kanuni za bunge.mabadiliko yaliyopitishwa yataanza kutumika mara moja.

(2) Iwapo jambo au shughuli yeyote haikuwekewa masharti katika kanuni hizi,Spika

ataamua desturi na utaratibu wa kufuatwa katika jambo au shughuli hiyo.

46. Kanuni hizi zitatumika katika mkutano wa Bunge uliozipitisha mara baada ya kupitisha hivyo.

47. bila kuathili mashariti ya kanuni hizi ,iwapo muda wa kuanza kikao umefika basi wabunge waliopo watapiga kura ya kuendelea na kikao au kutoendelea ,na mamuzi yatakayofanyika yatakuwa halali